
# NIMEINGIA MAHALI HAPA

E . I . Kalluh
Mwanza-1986



S./A.



1. Makao yako yapendeza sana, Ee Bwana Mungu wa Majeshi
Nakipenda kikao cha nyumba yako, Na mahali pa hema ya utukufu wako.

2. Nalifurahi waliponiambia tutaingia nyumbani mwa Bwana,
Sasa miguu nyetu imesimama katika milango yako ee Yerusalemu

3. Ingieni mlangoni kwa kumsifu Bwana,
Nyumbani mwake tumtolee shime, tutukuze jina lake.

4. Dunia nzima imshangilie Bwana,
Kwa furaha tumtumikie wote, tumwendee na nyimbo za shangwe.

5. Ee Mungu wangu, Mwumba wangu, uwe furaha yangu,
Nikutumikie kwa moyo mkunjufu mimi mwanao.

6. Unipe ushindi juu ya adui zangu,
Usiniache kupotoka na kulemewa na shetani.

7. Mwanga wako na ukweli wako viniongoze ee Bwana,
Vinifikishe kwenye maskani yako yenye utukufu wa milele.